BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Kumi – Tarehe 02 Oktoba, 2018.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

I. TAARIFA YA SPIKA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Waziri wa Fedha na Mipango:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Wizara ya Fedha na Mipango ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC) kwa mwaka 2017/2018.

Waziri wa Fedha na Mipango:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Wizara ya Fedha na Mipango ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Bajeti kwa mwaka 2017/2018.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC):

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC) Kuhusu Ripoti ya Wizara ya Fedha na Mipango ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC) kwa mwaka 2017/2018.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti:
Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Bajeti Kuhusu Ripoti ya Wizara ya Fedha na Mipango ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Bajeti kwa mwaka 2017/2018.

III. MASWALI:

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

79. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kwa muda mrefu njia ya ndani ya Jambiani ni mbovu na inaleta usumbufu kwa wananchi. Aidha, wagonjwa na wajawazito inakuwa vigumu kufikishwa vituo vya afya lakini pia njia hiyo ndiyo inayotumiwa na watalii kwenda kwenye hoteli nyingi zinazopakana na njia hiyo.

(a) Je, Serikali ya Halmashauri ya Wilaya ya Kusini lini itachukuwa hatua za makusudi na za haraka kuitengeneza njia ile kwa kiwango cha lami ili kunusuru hali ya kijamii na kiuchumi katika eneo la Jambiani.

(b) Je, Serikali haioni kuacha njia hiyo kuwa mbovu hasa kipindi cha mvua, inarudisha nyuma shughuli za kiuchumi za wananchi na harakati za utalii ambao unachangia pato la taifa.

(c) Je, Wizara ipo tayari mara baada ya kujibu swali hili kufuatana na Mwakilishi kwenda kuikagua njia hiyo na kufanya tathmini ya matengenezo yake.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

59. MHESHIMIWA SAADA RAMADHAN MWENDWA (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Serikali imekuwa ikitoa kipaumbele cha elimu kwa vijana hasa watoto wa kike ili kutekeleza dhamira ya muasisi wa Mapinduzi na Rais wa Kwanza wa Zanzibar, Mzee Abeid Amani Karume. Pamoja na dhamira hiyo nzuri, bado lipo tatizo la vijana wa kike kukatizwa masomo yao kutokana na kupata ujauzito wakiwa masomoni.

(a) Je, ni vijana wangapi wa kike wa skuli za msingi na sekondari kwa mwaka 2017/2018 walikatisha masomo kwa kupata ujauzito.

(b) Je, ni hatua gani zimechukuliwa kwa wale waliowapa mimba vijana hao wa kike.

(c) Je, kuna kesi yoyote Mahakamani kutokana na kadhia hiyo.

Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:

6. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje): - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:

Kumekuwa na malalamiko kwa baadhi ya wananchi wanaokodishwa nyumba za maendeleo Michenzani kuwa wanalipishwa madeni ya nyuma ambayo wapangaji wapya hayawahusu. Suala hilo linaonekana wanafanyiwa baadhi ya watu kwa asili zao hali inayoonekana kama ni ubaguzi.

Je, kwanini Shirika la Nyumba linawalipisha wateja madeni ya nyuma kibaguzi na ambayo mpangaji mpya hayamuhusu.

7. MHESHIMIWA Jaku Hashim Ayoub (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:

Matangi ya mafuta yaliyopo Wesha Kisiwani Pemba yamekodishwa kwa Kampuni ya GAPCO.

(a) Je, kwa mujibu wa mkataba wa ukodishwaji huo, matangi hayo yamekodishwa kwa miaka mingapi.

(b) Je, Kodi ya kiasi gani inalipwa Serikali kwa mwezi.

Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

129. MHESHIMIWA OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

Kwa kuwa Serikali imewataka wananchi waliokuwa na eka 3 ambazo hawakuwa na hati rasmi za matumizi hasa kwa mashamba ya mikarafuu, Pemba kuomba hati za eka hizo. Na kwa kuwa wananchi wameshaomba hati za mashamba hayo waliokuwa wakiyaendeleza kwa miaka 10 hadi 20 na walishapanda miti ikiwemo mikarafuu.

(a) Je, hadi sasa ni hati ngapi zilizotoka kwa ajili ya wananchi walioomba hati za eka 3 hasa kwa shamba za mikarafuu Pemba.

(b) Je, hadi sasa kuna maombi mangapi ya wananchi ambao wameomba shamba za eka 3 ambao bado hawajapatiwa.

(c) Je, ni lini Serikali itawapa wananchi walioomba hati hizo ukitilia maanani wimbi kubwa la ukataji mikarafuu kupigia tanu za mkaa baada ya wananchi waliokuwa wakiyatunza kuyaacha kwa sababu ya kutokupatiwa hati.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

107. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimwia Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji.

Kisiwa cha Zanzibar kina watu wachache na vyombo vya moto vichache, lakini kuna ajali nyingi baadhi zikisababishwa na uzembe au hata kufanywa kwa makusudi kwa madereva kuendesha mbio kupita kiasi au kutotii sheria za barabarani.

(a) Je, ni sababu zipi zinazosababisha kutokea kwa ajali zinazojirudia mara kwa mara.

(b) Je, umeshawahi kufanywa utafiti wa ajali na ikaonekana tatizo ni nini.

Wizara ya Afya:

17. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB ((Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Zanzibar ni visiwa na kwa bahati mbaya hakuna mpango wa kudhibiti uingiaji holela wa watu kutoka nje ya visiwa, tofauti na visiwa vingi duniani kama vile ambavyo vimo kwenye muungano kama Hongkong. Hivi karibuni kumeripotiwa kesi nyingi za ongezeko la maambukizi ya ukimwi hasa kwa wageni wanaongia.

(a) Hali ya maambukizi ya ugonjwa wa ukimwi ikoje Zanzibar kwa hivi sasa.

(b) Kwanini Zanzibar haina udhibiti wa uingiaji wa watu kiholela ukizingatia hivi ni visiwa vyenye rasilimali chache na eneo dogo na haliwezi kuhimili hali ya maambukizi ya ukimwi na magonjwa mengine.

(c) Wizara imechukua hatua gani kuishauri Serikali kupitia taasisi mbali mbali za Serikali kudhibiti hali hatarishi kama kuongezeka maeneo ya starehe na madanguro, ambayo yanahusiana na ongezeko la vitendo vya uasharati ambavyo ni chanzo kikubwa cha maambukizi ya virusi vya UKIMWI.

Wizara ya Biashara na Viwanda:

20. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Viwanda:

Jumuiya ya Wafanyabiashara wenye Viwanda na Wakulima Zanzibar (ZNCCIA) ni mwamvuli mkubwa wa wafanyabishara na kielelezo cha sekta binafsi inayosaidia katika maendeleo ya nchi. Kwa muda mrefu, Jumuiya hii imekuwa haifanyi shughuli zake kiufanisi kwa sababu mbali mbali.

(a) Kutokana na Jumuiya hii mpaka sasa kutokuwa vizuri katika usimamizi wake. Je, Wizara imechukuwa hatua gani kuwaita na kuwashauri.

(b) Kwanini Ofisi ya Jumuiya hiyo Kisiwani Pemba imefungwa wakati ile ya Unguja muda wote ipo wazi.

(c) Tangu kuchaguliwa Mwenyekiti mpya wa Jumuiya, kuna vikao vingapi vimefanyika na Wizara wamealikwa kwenye vikao hivyo.

37. MHESHIMIWA OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Viwanda:

Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) ni shirika linalojiendesha kibiashara. Na kwa kuwa zipo fursa nyingi za kibiashara Tanzania Bara zitakazoliwezesha shirika kujiongezea kipato kwa kununua na kusafirisha nje ya Tanzania bidhaa kama korosho, kahawa, ufuta, mbaazi, dengu pamoja na kuanzisha kiwanda cha kuzalisha mafuta ya alizeti ambayo inalimwa Tanzania Bara.

Je, Shirika la ZSTC lina mpango gani wa kuzitumia fursa za mazao ya kilimo kwa kuvisarifu au kuvifungasha na kusafirisha nchi za nje kuliko kusubiri wakati wa msimu wa mavuno ya karafuu pekee.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

Waziri wa Fedha na Mipango:

Ripoti ya Wizara ya Fedha na Mipango ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC) kwa mwaka 2017/2018.

Waziri wa Fedha na Mipango:

Ripoti ya Wizara ya Fedha na Mipango ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Bajeti kwa mwaka 2017/2018.

Zanzibar,
02 Oktoba, 2018.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA.